

Utandawazi wa Kiswahili: Mitazamo ya Ukubalifu na Mkwamo kama Lugha Rasmi ya Afrika

Gerephace Mwangosi

Idara ya Lugha, Chuo Kikuu cha Kikatoliki Ruaha

Email: *mwangosigerephace@yahoo.com*

Ikisiri

Matilaba ya makala haya ni kueleza mambo yaletayo mielekeo tofauti ya watu kuhusu upokezi na matumizi ya lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi ya Afrika ili kushurutisha ukubalifu wake. Aidha, yanabainisha baadhi ya masuala yanayotiliwa shaka kuhusu uwezo wa lugha ya Kiswahili kumudu harakati na mahitaji ya utandawazi, kama vile, katika kupitisha teknolojia mpya inayoinukia katika nyanja za sayansi na teknolojia. Kwa jumla, makala haya yanauia kufafanua ukubalifu, pamoja na msingi wa mielekeo ya Waafrika kutoipa kipaumbele lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi ya bara lao.

Maneno ya Msingi: Kiswahili, utandawazi, ukubalifu, mkwamo na sera.

Utangulizi

Lugha ya Kiswahili, kama zilivyo lugha nyingine za dunia, kama vile; Kiingereza, Kijerumani na Kiarabu, imepiga hatua kubwa, na kuwa moja ya lugha za mataifa kwa minajiri ya kupanua na kuimarisha mahusiano ya kimataifa katika nyanja zote za kijamii. Hatua za kuendelea kukua na kupanuka kwa lugha ya Kiswahili kimatumizi na kijiografia, ni mojawapo ya jitihada za kutozitenga nchi za Kiafrika katika jamii za kimataifa. Aidha, kwa kuwa utandawazi unahusika na uunganishaji wa mataifa mbalimbali, basi Afrika nayo inahitaji lugha moja yenye asili ya Kiafrika kama lugha ya kuusambaza na kuukabili utandawazi. Kwa sasa, lugha ya Kiswahili ni mfano mzuri wa lugha kwa kuwa ina historia ndefu kama lugha kubwa barani Afrika.

Utandawazi wa Kiswahili, Historia na Maendeleo yake

Kulingana na Sullivan (1994) pamoja na Little (1996), utandawazi ni dhana inayolenga katika kupunguza na hata kuondoa mamlaka ya dola katika nchi kwa kuzidisha mamlaka ya mashirika ya kimataifa ili kudhibiti uwezo wa mashirika ya kitaifa. Utandawazi

[Ruaha Journal of Arts and Social Sciences Vol 2, 2016](#)

una dhamira ya kuondoa vikwazo vyote vya kijiografia na kisiasa ili kuruhusu mtiririko huru wa nguvu kazi baina ya mataifa. Maelezo haya yatumika kama msingi wa kupima nguvu na mtiririko wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya utandawazi ndani na nje ya bara la Afrika.

Aidha, utandawazi ni dhana inayotumiwa kuelezea mikabala ya kiutamaduni, kielimu na hata kisiasa inayosisitiza maungano na mahusiano yanayokiuka mipaka ya taifa moja na jingine, pamoja na kuenea na kusambaza tamaduni kutoka sehemu moja hadi nyingine. Utandawazi husambazwa kupitia itikadi, teknolojia na lugha (Amatubi, 2002). Kwa hiyo, lugha ndicho chombo muhimu zaidi katika usambazaji wa utamaduni. Hapa Afrika, kama ilivyokwisha fafanuliwa, Kiswahili ndiyo lugha muafaka ya kuijenga kijiografia na kimatumizi ili kuukabili utandawazi.

Kwa namna hali ilivyo sasa, hapana shaka kuwa utandawazi umeenea katika bara la Afrika kupitia lugha za kigeni, mfano, Kiingereza na Kifaransa. Hali hii yafaa kutupiliwa mbali iwapo bara la Afrika linatarajiwa kunufaika kikamilifu kutokana na utandawazi (Njihia, 2005). Aidha, kwa vile utandawazi unahusika na uunganishaji wa mataifa mbalimbali, basi Afrika yahitaji lugha moja yenye asili ya Kiafrika, kama lugha ya kuusambaza utandawazi. Kwa sasa, lugha ya Kiswahili ina historia ndefu, na ni wakati muafaka wa kuijenga, kuikuza na kuikomaza kimatumizi ili kuukabili utandawazi. Kwa jumla, lugha ya Kiswahili ilianza kuwa lugha ya kimataifa na kuwekwa katika ramani ya utandawazi kupitia biasharaya watumwa, baina ya Afrika Mashariki, mataifa ya Uarabuni pamoja na yale ya Ulaya.

Utandawazi wa Kiswahili ulianza kabla na baada ya kuteuliwa mwaka 1925 kuwa lugha rasmi ya Afrika Mashariki, ambapo uteuzi huo uliambatana na zoezi la usanifishwaji wake (Mbaabu, 2007). Kwa upande mwingine, utandawazi wa Kiswahili unajipambanua katika historia na asili yake iliyofungamana na nadharia za kiisimu na kihistoria ambazo zinathibitisha kupitia ubantu wake, na mwingiliano wa muda mrefu baina ya jamii za ndani na nje ya Afrika Mashariki (Guthrie, 1948). Matokeo yake, lugha ya Kiswahili ilianza kuvunja mipaka ya kijiografia, kimatumizi na kimsamiati hata kabla ya ujio wa Wakoloni kutoka bara la Ulaya.

Ujio wa Wamisionari katika Afrika Mashariki ulisaidia sana kutandawazisha Kiswahili. Wamisionariwalianza kuifundisha lugha ya Kiswahili katika mataifa ya Magharibi, na ndio waasisi wa somo la Kiswahili katika vyuo vikuu katika nchi za Magharibi, kwa mfano, Leiden nchini Ujerumani (Sapir,1958). Aidha, shughuli za vyombo vya habari zimechangia sana kuisambaza lugha ya Kiswahili ulimwenguni kote kutokana na kuwepo kwa idhaa maarufu za utangazaji duniani, baadhi yake ni BBC (London) na VOA (Marekani). Pia, zipo redio, magazeti na majarida yanayochapishwa kwa lugha ya Kiswahili katika mataifa ya Magharibi na Mashariki.

Jambo lingine linaloithibisha utandawazi wa lugha hii, ni namna inavyowianishwa na lugha nyingine barani Afrika. Kwa mfano, hapa ulimwenguni Afrika ndilo bara linalofikiriwa kuwa na lugha nyingi kuliko mabara mengine, ambapo linakadiliwa kuwa na lugha kati ya 800 na 1140 (Bourhis, 1982). Katika lugha hizo, Kiswahili, Kihansa na Kiarabu, ndizo lugha zenye wasemaji wengi kuzidi hata baadhi ya lugha za kigeni, kama vile; Kijerumani, Kireno na Kifaransa. Lugha ya Kiswahili imeweza kuvuka mipaka ya utafu wa mataifa ya Afrika Mashariki, kiasi cha kuteuliwa kuwa lugha rasmi ya umoja wa Afrika tangu mwaka 1986, na mwaka 2004 ilianza kutumika rasmi. Kuchelewa kwa utekelezaji wa azimio hilo pengine kumetokana na kukosekana kwa sera makini zinazolenga kuikuza na kuiendeleza (Mekacha, 2000). Kwa jumla, lugha ndicho chombo mahususi cha kuwaunganisha watu katika kutekeleza majukumu yao katika nyanja zote za kijamii. Afrika, haina budi kukuza na kuzitumia lugha zake.

Mitazamo ya Wasomi Kuhusu Utandawazi wa Kiswahili

Ryan na wenzake (1982) wanafafanua kuwa mitazamo ya lugha, kwa upana wake, ni ukadiriaji wowote wa kihisia, kiufahamu na kitabia kuhusu mwitikio wa wazungumzaji wa lugha inayohusika. Jambo linalosisitizwa katika ufafanuzi wa mitazamo, ni ile hali ya kuwa tayari kiakili na kuitumia lugha katika nyanja zote za kijamii. Kwa hiyo, mitazamo huonesha hisia za kupenda au kutopenda kitu fulani. Kwa jumla, suala la mitazamo kuhusu lugha ya Kiswahili linahitaji kuwekwa dhahiri zaidi.

Kwa upande mwingine, mitazamo ya lugha hujumuisha umuhimu wa kijamii unaoambatanishwa na lugha, pamoja na namna mbalimbali za matumizi ya lugha katika jamii. Umuhimu wa lugha ni miongoni mwa mambo yanayochangia mitazamo ya lugha. Aidha, lugha yenye watu wengi katika shughuli nyingi na muhimu, watu huipa umuhimu wa kujenga mitazamo chanya kwake. Edwards (1982) anasisitiza kuwa kwa kawaida lugha iliyo na hadhi, na ambayo imepata maenezi mapana, itakuwa na mtazamo chanya inapolinganishwa na lugha nyingine ndogo kimatumizi. Kwa mfano, lugha ya Kinyakyusa ina hadhi ndogo ikilinganishwa na Kiswahili, na lugha ya Kiswahili ina hadhi ndogo kikilinganishwa na ile ya Kiingereza. Hoja hii ndiyo inayoibua mitazamo chanya na hasi kuhusu uwezo wa lugha ya Kiswahili kutumika kama lugha ya bara Afrika.

Licha ya hadhi, umuhimu wa lugha huchangiwa pia na wazungumzaji wa asasi zinazoiunga mkono. Hadhi ya lugha hujumuisha nguvu za kiuchumi, kisiasa na kijamii, pamoja na matumizi katika viwango vya elimu, idara za serikali kitaifa, kimaeneo, kibiashara, uchapishaji na matumizi mapana katika vyombo vya habari (Triands, 1971). Kwa hiyo, ipo mielekeo ya ukubalifu wa lugha ya Kiswahili barani Afrika katika kipindi hiki cha utandawazi.

Ukubalifu wa Utandawazi wa Kiswahili

Kiswahili ndiyo lugha ambayo inaukubalifu wa kimataifa kuliko nyingine barani Afrika kwa sababu ina usilimisho unaorahisisha kujifunza na kuitumia, na ni lugha inayoweza kuzimudu teknolojia mpya zinazoibuka kupitia uundaji wa maneno (Ryanga, 2002). Suala hili la utandawazishwaji wa lugha katika nchi changa na zinazoinuka kiuchumi, tayari nchi nyingi zimeanza kwa dhati kutandawazisha lugha zao za kiasiliili zinufaike kikamilifu katika mfumo wa utandawazi. Baadhi ya mataifa hayo ni Israel, China, Japan na Korea. Kwa hiyo, bara la Afrika linapaswa kuiga mataifa haya na kuanzakutandawazisha kwa vitendo lugha zake za kiasili ili kuukabili utandawazi, kama inavyofafanuliwa na Chachage (2003):

Bara la Afrika litaingia katika utandawazi kupitia juhudi pana za kujitegemea na kuondoa umelea wa kutegemea lugha za kigeni kimsamiati na katika nyanja zote za kijamii.

Kwa hiyo, ipo hoja ya kubadilisha mitazamohasi kuhusu lugha za Kiafrika, hasa lugha ya Kiswahili ambayo iliteuliwa kuwa lugha rasmi ya Afrika tangu mwaka 1986, na kuanza kutumika mwaka 2004. Hakuna taifa lililopiga hatua katika nyanja za kiteknolojia na kiuchumi kwa kutumia lugha za kuazima. Mataifa ya Afrika yana wajibu wa kuikuza, kuikomaza na kuipanua kijiografia na kimatumizi lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, Pono (2001) anatoa angalizo kuwa, siyo lazima tuyaue matumizi ya lugha za kigeni ili tukuze kiswahili kama lugha ya Afrika.

Kukwama Kwa Utandawazi WA Kiswahili

- **Kasumba ya Kutawaliwa**

Kasumba za kikoloni pamoja na sababu za kihistoria zimesababisha kwa kiasi fulani kuwepo kwa mielekeo tofauti tofauti kuhusu lugha ya Kiswahili. Tangu tupate uhuru kuna mivutano katika jamii za Kiafrika zilizotawaliwa na Wazungu. Kwa mfano, kuna wale wanaodai kuwa lugha za Kikoloni ni vigezo muhimu vya kupimia hadhi ya mtu kijamii, kiuchumi na kitaifa. Mtazamo huu unaangukia katika kuzienzi lugha za Kikoloni na unaambatana na jitihada kubwa za kuzipuuza lugha za kiasili za Kiafrika, na kuiona katika uchanga usioweza kumudu mahitaji ya utandawazi barani Afrika, ikiwemo lugha ya Kiswahili (Bourhis, 1982). Pamoja na jitihada zao za kibinafsi, lugha hizo zimesalia kuwa za watu wachache sana.

Aidha, kasumba za kikoloni zimeambatana pamoja na baadhi ya wasomi wanaoamini kuwa Kiingereza ni lugha ya sayansi na teknolojia, na ni alama ya usomi (Qorro, 2002). Mwelekeo huu ndio unaozifanya lugha za Kiafrika kuonekana kama lugha ambazo haziwezi kumudu mahitaji katika elimu ya juu, sayansi na teknolojia za kigeni. Kwa hakika, teknolojia hizo zinaendelea kubaki nje ya utamaduni wa jamii za Kiafrika kwa sababu lugha zinazotumika kufundishia hazieleweki kwa walimu, wanafunzi na wananchi walio wengi. Tathmini sahihi ya kushuka kwa lugha, lazima Kiingereza kiangaliwe kama pingamizi la uelewa wa

[Ruaha Journal of Arts and Social Sciences Vol 2, 2016](#)

maarifa. Kwa hiyo, bara la Afrika halina budi kutumia lugha zake za asili ili kuepuka utegemezi wa lugha za kigeni, ambao, kwa hakika, hauna tija kwa maendeleo na ustawi wa watu wake.

Kwa mujibu wa Ansre (1977), wasomi wa bara la Afrika wameathirika kisaikolojia kutokana na kukomaa kwa kasumba za kigeni. Athari kubwa ya tatizo la kisaikolojia ni kutojiamini. Suala la kutojiamini ndilo linalosababisha baadhi ya wasomi kufikiri kuwa lugha zetu hazina maana wala mchango wowote katika ulimwengu wa kisasa, na kuziendeleza ni kama hatua ya kurudi nyuma. Pia, wanaona kama utamaduni wetu una hitilafu na kuwa maendeleo ya sayansi na teknolojia ni mambo ya Wazungu. Hivyo, hatuna budi kuiga yote ili kupata teknolojia ya haraka kwa kutumia lugha zilizoendelea kisayansi na kiteknolojia. Crystal (1992) anaukosoa mtazamo huo kuwa waneni wa lugha ya kwanza au lugha ya mama hujihisi kuwa salama na hujivunia lugha zao. Afrika haina budi kutumia lugha zake kwa manufaa ya maendeleo yake.

Kwa jumla, hali ya kutojiamini ndiyo inayowafanya wasomi na wanasisia kuwa na mijadala isiyoisha na inayopuuza harakati za Kiswahili kutumika kufundishia elimu ya juu. Kuhusiana na hili, Birgit Brock-Utne (2000) anasema kuwa lipo tatizo la kuziona lugha za Kiafrika kama zenye upungufu badala ya kuziona kama rasilimali. Jambo hili ni kinyume na matakwa ya maisha ya ulimwengu wa sasa. Matokeo ya hali hiyo ni kudumaa kwa utamaduni wa Kiafrika. Hapa ikumbukwe kwamba hata mataifa ya Ulaya yalipokea sayansi na teknolojia kutoka katika utamaduni wa Wayunani, Wamisri na Wagiriki, na kuumiliki kikamilifu kwa kutumia lugha zao. Haya yanawezekana kwa kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya Afrika.

- **Ukosefu wa Sera ya Lugha**

Kukosekana kwa sera ya lugha ndio msingi mkuu wa kusuasua kwa hadhi ya Kiswahili kama lugha rasmi barani Afrika. Licha ya Kiswahili rasmishwa tangu mwaka 1986, mpaka sasa hakuna sera zinazolenga kuijenga, kuikuza na kuiendeleza (Msanjila na wenzake, 2009). Kwa hiyo, jambo la msingi hapa ni kwamba, sera kama mwongozo wa mpango na utekelezaji, ni muhimu kuandaliwa, kuidhinishwa na kutumika. Kiswahili kama lugha

[Ruaha Journal of Arts and Social Sciences Vol 2, 2016](#)

rasmi ya Afrika haiwezi kustawi na kuhimili harakati za utandawazi kama itakosekana sera ya lugha inayolihusisha bara zima.

Katika muktadha wa Afrika, Kiswahili ndiyo lugha rasmi. Kwa hiyo, uundaji upya wa sera za lugha katika nchi za Kiafrika unafaa kujumuisha lugha za Kiafrika kutokana na mahitaji ya kimataifa (Msanjila, 1997). Msimamo wa pamoja kuhusu chaguo la lugha kimaeneo, utachochea mtazamo endelevu katika kila nchi, na hivyo kufikia malengo ya Kiswahili kutekeleza shughuli za umoja wa Afrika na kuukabili na utandawazi.

- **Udhaifu wa Asasi za Kutandawazisha Kiswahili**

Ukuzaji wa lugha katika uwanja wa maarifa mapana na ya kina unahitaji vitendea kazi vinavyokidhi mahitaji ya kimatumizi kwa kuzingatia mawanda yake kijiografia. Barani Afrika, upatikanaji wa vitendea kazi ni tatizo kubwa linalotokana na utegemezi kutoka nje, ambavyo, kwa hakika, vimeandaliwa kwa ajili ya mazingira yao. Aidha, hakuna chombo madhubuti kilichoundwa ili kusimamia ukuzaji wa Kiswahili barani Afrika. Kwa mfano, Katiba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (2000: kifungu 137) inaeleza kwamba, Kiingereza ndiyo itakayokuwa lugha rasmi ya Jumuiya, na lugha ya Kiswahili itakuzwa kama lugha ya mawasiliano mapana. Hali hii, inaviza na kuvunja nguvu za msukumo wa kukazania matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi ya Afrika.

Pia, kukosekana kwa vyombo imara vya kukuza lugha ya Kiswahili, ambavyo, kimsingi vipo kijiografia na kinadharia zaidi, kwa mfano, BAKITA, BAKIZA, CHAKA, TATAKI na TAKILUKI. Uzoefu unaonesha kuwa havijafanikiwa kutekeleza wajibu wao kikamilifu kwa sababu ya ukosefu wa fedha pamoja na kutazamwa kama vyombo vya kitaifa na kikanda. Kwa upande mwingine, ipo mikakati na hatua za makusudi zinazofanywa na mashirika ya kimataifa, kama vile, Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la kimataifa kutotoa huduma iwapo lugha ya Kiswahili itatumika. Nchini Tanzania na Uganda, shirika la misaada la Uingereza lilitoa msaada wa ukuzaji na uimarishaji wa Kiingereza kwa masharti, ambapo nchini Uganda yalitishia misaada yao iwapo nchi hiyo ingeamua kufundisha Kiswahili (IMF, 1997).

[Ruaha Journal of Arts and Social Sciences Vol 2, 2016](#)

Matatizo haya, yanatokana na mwelekeo wa kisiasa na kasumba ya kutawaliwa. Mitazamo chanya ya mabadiliko kama hayo ikitokea, lugha za asili za Kiafrika zitapewa nafasi zinazostahili (Mhina,1977). Haya ndiyo matarajio ya wengi.

Mapendekezo

Bara la Afrika halina budi kutambua kuwa kila jamii ina maarifa yake ambayo ina wajibu wa kuyaendeleza na kuyaboresha kwa mawanda mapana ili yaendelee kubuniwa na kupanuliwa kwa kutumia lugha zake. Utambuzi huu ukiwepo utaweka msingi mahususi wa kukuza maarifa ya jamii yake, pamoja na kuvipa fursa vigezo vya upangaji lugha itakayotumika kuukabili utandawazi barani Afrika. Huu ni wakati muafaka kwa mataifa ya Afrika kuunda sera ya lugha inayohusisha mataifa yote na kuzitekeleza kwa vitendo. Uzoefu uliokwishaonekana barani Afrika kuwa Kiswahili ndio lugha muafaka yenye asili ya Afrika inayoweza kuzimudu harakati za utandawazi. Mataifa ya Afrika yana wajibu wa kuikuzi na kuipanua kijiografia na kimatumizi.

Hitimisho

Mataifa ya Kiafrika yanatumia lugha za kigeni na yanatofautiana kisiasa kutegemea watawala waliozitawala nchi hizi. Kwahiyo, utamaduni wa mataifa ya Afrika hauna uwiano wa kufikia kuwa na sera ya lugha moja. Aidha, mapinduzi ya kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia katika mataifa yanayoendelea na yaliyoendelea, kwa mfano; Urusi, Marekani, Uingereza, Ufaransa na Ujerumani yanahusishwa moja kwa moja na matumizi ya lugha zao za asili, na si za kuazima kama ilivyo barani Afrika. Kwa hiyo, ni wakati muafaka kwa mataifa ya Afrika kuunda sera ya lugha inayohusisha mataifa yote na kuzitekeleza kwa vitendo. Kwa kufanya hivyo, lugha ya Kiswahili itakuwa alama ya Uafrika katika kuukabili utandawazi.

Marejeleo

Ansre,G.(1977).Four Rationalizations for Maintaining the European Language in Education in Africa.In Kiswahili 47/2:55-61

Brock-Utne, B. (2000). *Whose Education for All? The Recolonization of the Africa Mind*. Falmer, New York

[Ruaha Journal of Arts and Social Sciences Vol 2, 2016](#)

- Bourhis, R. Y. (1982). *Language Policy and Language Attitudes*.
Katika Ryan, E. B. and Giles, H. (1982). *Attitudes Towards
Language Variation*. Edward Arnold, London
- Chachage, S.C. (2003). *Kiswahili katika Muktaba wa
Utandawazi*. BAKITA
- Crystal, D. (1992). *An Encyclopedic Dictionary of Language and
Language*. MA: Blackwell, Cambridge
- Edwards, J. R. (1982). *Language, Society and Identity*. Basil
Blackwell, Oxford
- Edwards, J. R. (1985). "Language Attitudes and Their
Implications Among English Speakers", katika: Ryan,
E. B. and Giles, H. (1982). *Attitudes Towards Language
Variation, Social and Applied Contexts*. Edward
Arnold, London
- Guthrie, A. (1948). *The Classification of the Bantu Languages*.
O.U.P. London
- International Monetary Fund (1997). *World Economic. I. M. F,
Outlook*
- Little, A. (1996). *Globalization and Education Research: Whose
Context Counts? International Journal of Development
Vol.16, No.4. 427 – 438*
- Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. TUKI
- Mekacha, R.D.K. (2000). *Isimujamii: Nadharia na Mktadha wa
Kiswahili*. Osaka University of foreign studies
- Mhina, G. (1977). *The Tanzania Experience in the Use of
Kiswahili in Education*. In *Kiswahili* 47/2:6 – 69
- Msanjila, Y. P na Wenzake, (2009). *Isimujamii*. TUKI

- Msanjila, Y. P. (1997). "Towards a Policy on the Use of Kiswahili in Africa" katika Kiswahili Juzuu la 60, TUKI
- Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Educational Publisher and Distributors Ltd, Kibaha
- Njihia, S.K.(2005). Kiswahili na Utandawazi, katika Insha za Jubilei 2005, Utandawazi na Umoja wa Afrika. TUKI
- Qorro, M. (2000). Mjadala wa lugha ya kufundishishia: sababu zinazotolewa kupitia matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia. *Katika* J.S. Mdee na H.J.M Mwansoko (Waherini) Kiswahili 2000 Proceeding. TUKI
- Rono, M. (2001). *We should Arise and Save Kiswahili: The People*, Nairobi.
- Ryan, E. B. (et.al) (1982). "An Intergrative Perspective for the Study of Language" katika *Attitude Towards Language Variation*. Edward Arnold, London
- Ryanga, S. (2002). "The African Union in the Wake of Globalization: The Forgotten Language Dimension" *katika* Kiswahili Juzuu 65 Dar, TUKI, UK. 1-15
- Roy-Campbell and Qorro, M. (1997). *The Language Crisis in Tanzania: The Myth of English Versus Education*. Mkuki na Nyota, Dar
- Sullivan, T. (1994). *Key Concepts in Communication and Cultural Studies*. Routledge Press, Canada